

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



Mtaa wa Mahakama,
S. L. P. 1419,
53103 MBEYA.
Simu: (025) 252503566
Nukushi: (025) 252502958
Barua pepe: rbcmbeya@pccb.go.tz
Wavuti: <http://www.pccb.go.tz>

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**TAARIFA YA KUKAMATWA
MTUMISHI WA TAZARA MBEYA**

Ndugu wanahabari,

Napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru wote kwa kuitikia wito wetu, pia niwapongeze kwa kazi nzuri mnayoendelea kuifanya ya kutoa habari na kuelimisha umma wa Watanzania.

Nimewaita leo kwa ajili ya kutoa taarifa kuhusu kwa Bw. Bahati Selemani ambaye pia anajulikana kwa jina la Rashid Abedi Mwakipili - mtumishi wa mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia - TAZARA mkoa wa Mbeya.

Bw. Bahati atafikishwa katika Mahakama ya Hakimku Mkoani Mbeya kwa kosa la kupokea rushwa ya Tsh. 200,000/= kinyume na kifungu cha 15 cha sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007.

Awali ilidaiwa kwamba, siku ya tarehe 11/02/2019 Bw. Bahati alidai fedha kiasi cha shilingi 400,000/= kutoka kwa mfugaji wa Ng'ombe ambaye alimkamata kwa kosa la kulisha ng'ombe wake katika eneo la hifadhi ya Reli lililoko Chimala wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, ili asimchukulie hatua kwa kosa hilo.

Mshitakiwa alikamatwa na TAKUKURU siku ya tarehe 12/2/2019 akipokea hongo ya Tsh. 200,000/= ambazo ni sehemu ya fedha aliyoomba.

Ndugu wanahabari,

Nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wote wa mkoa wa Mbeya ambao wanaendelea kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa katika mkoa wa Mbeya katika Mapambano dhidi ya Rushwa.

Nazidi kuwasihii wananchi waendeleo kutuunga mkono kwa kutupatia taarifa ya vitendo vya rushwa kwa kuleta taarifa ofisini au kuwasiliana nasi kwa njia ya SIMU YA DHARURA nambari 113 BURE kwa kupiga au kutuma ujumbe mfupi wa maneno. Vilevile unaweza kutuma taarifa kwa kubonyeza *113# na kufuata maelekezo.

Baada ya kusema hayo, nawashukuruni sana kwa kunisikiliza.

JULIETH MATECHI
Kny: MKUU WA TAKUKURU MKOA WA MBEYA
FEBRUARI, 2019
